# Maelezo ya Kitkit shule

Kujifunza kidijitali kulikotengenezwa kwa ajili ya kushirikisha na kuwezesha

## Tumetengeneza Kitkit shule ili kuleta uzoefu wa hali ya juu wa kujifunza kwa watoto wenye uhitaji zaidi duniani kote

Jina lake likitokana na neno "Kufikiri" kwa lugha ya Kithai, Kitkit shule ni utatuzi mpana wa mafunzo ya awali ikiwa na mtaala unaoanzia utotoni hadi elimu ya msingi. Kitkit shule imeunganisha mazoezi bora ya kimataifa kwenye kusoma, kuandika na kuhesabu pamoja na muundo sawa wa kanuni za kujifunza **kumsaidia kila mtoto kufanikiwa kama mwanafunzi huru.** Usanifu wa kujifunza unaoweza kubadilika wa Kitkit shule unakuja na uzoefu wa mtumiaji unaovutia na mrahisi kutumia ambao **unashinda mipaka ya kitamaduni na kuleta matokeo chanya kwa wanafunzi wote duniani.**

Kitkit shule inajumuisha michezo midogo midogo, vitabu, video, nyimbo, na majaribio ambayo yanawasaidia watoto kujifunza kusoma, kuandika, kuhesabu na matendo ya kihesabu. Program pia ina maktaba ambayo wanafunzi wanaweza wakaichunguza kwa uhuru. **Kama mshindi mwenza wa shindano la kujifunza duniani la Xprize**, Kitkit shule imeonyesha ongezeko kubwa na itakuwa program ambayo itakuwa inapatikana kwa ajili ya kila mtu mahali popote kuweza kutumia fursa za kielimu ambazo inatoa.

### KUJIBU HITAJI

Kwa mujibu wa UNESCO**, watoto wadogo pamoja na vijana milioni 617 duniani kote** - sita kati ya kumi hawajafikia kiwango cha ustadi kinachohitajika kwenye kusoma na kuhesabu. Pamoja[1] na hayo, watoto na vijana milioni 263 duniani kote hawapo[1] mashuleni. Wakati mifumo ya elimu kwenye nchi zinazoendelea imeongeza shule kwa kiwango kinachoridhisha katika miongo ya karibuni, kuna uhitaji wa haraka wa kuongeza ubora na kujifunza.

Katika kujenga bidhaa kuendeleza elimu ya kiwango cha juu kwa maisha yote, Enuma ilifanya majaribio Tanzania na Kenya kuangalia na kukusanya mrejesho, kutathmini maendeleo ya kujifunza na kuelezea jitihada zetu kwenye muendelezo wa uboreshaji. Kwa vile, tumeweza kuzifikia jamii, nchi, na mazingira ambayo yalikuwa ni magumu kufikika.

*Kujifunza zaidi kuhusu matokeo yenye nguvu ya Kitkit shule, tafadhali tazama muhtasari wetu wa matokeo.*

[1] UNESCO Institute for Statistics. (2017).

### TOFAUTI

Kitkit shule imeundwa na timu ya waundaji wa program za michezo na wakufunzi kuwezesha watoto WOTE, hasahasa walio katika mazingira magumu ambayo wanapata shida kwenye kujifunza.

Kitkit shule inawapatia wanaojifunza elimu ya awali ujuzi, kujiamini na mazoezi yanayohitajika kwenye kuondoa mwanya usioonekana uliopo kadri wana-vyotengeneza ujuzi wa msingi kwenye kusoma, kuandika na kuhesabu. Bila kujali uwezo wa mwan-zoni au upatikanaji wa shule, rasilimali na ushiriki-shwaji wa wazazi, Kitkit shule inawawezesha wanafunzi kuingia shuleni wakiwa na motisha na utayari wa kujifunza.

### KWA NINI KITKIT SHULE?

#### UJUZI WA MSINGI

Kujifunza kumetengenezwa kusaidia maendeleo na udadisi binafsi kadri mwanafunzi anavyojifunza kusoma, kuandika na hesabu

#### KUJIFUNZA BINAFSI

Ikiwa imetengenezwa kumlenga mtoto, na ikiwa na muonekano unaovutia inahakikisha kila mtoto anakuwa na uwezo wa kufanikiwa

#### UPATIKANAJI

Muonekano wa picha zenye mandhari ya asili na ufanyaji kazi unaopatikana kirahisi unawavutia na kuwawezesha wanafunzi tofauti tofauti duniani

Imeunganisha mazoezi bora ya kimataifa kwenye kusoma, kuandika na elimu ya hesabu ikiwa na muundo sawa kwenye kanuni za kujifunza, Kitkit iliundwa ili watoto wote waweze kuitumia binafsi na kujihisi kufanikiwa. Kitkit Shule ni bidhaa ambayo imeundwa kuzingatia mazingira ya dunia nzima ambayo inaweza ikachukuliwa kwa matumizi katika mazingira na lugha nyingine.



© 2019 Enuma, Inc. | Wasiliana nasi kwenye Kitkit@enuma.com

## YALIYOMO NDANI

KOZI **280** ZA KUSOMA NA KUANDIKA

KOZI **260** ZA HESABU

MAJARIBIO **260**




MAKTABA YENYE VITABU **130**


&


VIDEO ZA KUJIFUNZA **120**

**ZANA 8** KWA AJILI YA KUWEZESHA NA KUJIELEZA KIUBUNIFU

*Yaliyomo kwenye Kitkit shule toleo la 3(Yamesasishwa Novemba 2018)












## KUHUSU ENUMA INC.

Iliundwa mwaka 2012 ikiwa na malengo ya kuwawezesha watoto wenye mahitaji maalum kujifunza wenyewe, Enuma imefanya kazi kuweka viwango vipya kwenye uzoefu wa mtumiaji na upatikanaji wa muundo kwa ajili ya wanafunzi wa awali. Jina letu Enuma limetokana na neno enumerate, au kutaja mmoja mmoja, ambayo inaelezea dhamira yetu ya dhati kwenye mafanikio ya kila mtoto.

Imetengenezwa na watengenezaji wa program za kujifunza ambazo zimejishindia tuzo ikiwemo Todo Math, ambayo ni program nambari moja kwenye program za hesabu kwenye program zinazopatikana kwenye mfumo wa Apple, Kitkit shule ni matokeo yanayoonekana ya dhamira ya dhati ya Enuma kutoa  ufumbuzi wa kujifunza wenye kiwango cha juu kwa kila mtoto anayehitaji

*Mshindi mwenza, Shindano la kujifunza duniani la XPRIZE*

*Mmojawapo wa washindi, shindano la jiandikishe kwa changamoto ya kusoma na kuandika*

## SIFA ZA TABULETI INAYOSHAURIWA

Sifa za chini zinazohitajika kwenye tabuleti kwa ajili ya Kitkit ni

- Android Kitkat 4.4; 2GB RAM; Uwezo wa ndani 16GB
- Ukubwa wa kioo 1280 x 800
- Mwendelezo wa uwepo wa intaneti hautahitajika

## JIUNGE NASI

Wasiliana nasi kwenye Kitkit@enuma.com au tutembelee kwenye www.kitkitschool.com kujifunza zaidi kuhusu Kitkit Shule, matokeo yatu yanayokua, na kujadiliana kuhusu fursa za kujenga mahusiano



© 2019 Enuma, Inc. | Wasiliana nasi kwenye Kitkit@enuma.com